


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA



**Mkataba wa Kimataifa wa  
Kutokomeza aina zote za ubaguzi  
dhidi ya Wanawake wa Mwaka 1979:  
Ufafanuzi, utekelezaji wake Nchini  
Tanzania na tafsiri**

PARLIAMENT

BUNGE LA



## **DIBAJI**

Chapisho hili linatoa tafsiri ya Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa Mwaka 1979 (The Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women – CEDAW) katika lugha ya Kiswahili na kufanua namna Mkataba huo unavyoekelezwa nchini. Chapisho limeandaliwa na Bunge la Tanzania kuitia Awamu ya Pili ya Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (Legislative Support Programme (LSP II) katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na majukumu yao ili wayatekeleze kwa urahisi na ufanisi zaidi.

Hivyo, chapisho hili linazingatia umuhimu wa majukumu ya Bunge katika kulinda na kuendeleza haki za wanawake nchini na duniani kwa ujumla. Kwa kuzingatia umuhimu wa haki hizo, imeonekana kuwa ni vema Wabunge wakapata tafsiri ya CEDAW kwa lugha ya Kiswahili pamoja na ufanuzi wa utekelezaji wake katika muktadha wa Tanzania.

Kwa msingi huo, chapisho hili linatoa ufanuzi wa jumla kuhusu msingi wa haki za binadamu, chimbuko la Mkataba, wajibu wa Nchi wanachama, utekelezaji wa Mkataba nchini Tanzania pamoja na tafsiri ya kila Ibara ya Mkataba kwa lugha ya Kiswahili. Inatazamiwa kuwa, Wabunge na wasomaji wengine wa chapisho hili watajengewa uwezo wa kuulewa vema Mkataba huu na kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha kuwa ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake unakomesha na hivyo wanawake kupata haki zote kwa usawa na wanaume.

## **KANUSHO (DISCLAIMER)**

Tafsiri ya Mkataba huu imefanywa na Sekretarieti ya Bunge la Tanzania kwa lengo la kusaidia kujenga uelewa wa Mkataba wa Kimataifa wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka 1979 kwa Wabunge na Sekretarieti ya Bunge. Tafsiri hii isitumike kama tafsiri rasmi ya Mkataba huu, na wala isitumiwe na mtu ye yeyote nje ya utaratibu wa shughuli rasmi za Bunge la Tanzania

# **YALIYOMO**

|  |     |
|--|-----|
| <b>DIBAJI</b>  | i   |
| <b>KANUSHO (DISCLAIMER)</b>  | ii  |
| <b>YALIYOMO</b>  | iii |
| <b>SURA YA KWANZA</b>  | 1   |
| UFAFANUZI NA UTEKELEZAJI WA MKATABA NCHINI TANZANIA  | 1   |
| <b>1.0 UTANGULIZI</b>  | 1   |
| 1.1 Msingi wa Haki za Binadamu   | 1   |
| 1.2 Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu   | 1   |
| 1.2.1 Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 (The Universal Declaration of Human Rights, 1948) | 1   |
| 1.2.2 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966  | 2   |
| 1.2.3 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966                         | 2   |
| 1.2.4 Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Makundi Mbalimbali  | 2   |
| <b>2.0 MKATABA WA KIMATAIFA WA KUTOKOMEZA AINA ZOTE ZA UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE WA MWAKA 1979</b>           | 2   |
| 2.1 Chimbuko la Mkataba (CEDAW)  | 2   |
| 2.1.1 Hatua zilizochukuliwa na Tume  | 2   |
| 2.2 Mchakato wa Kutungwa kwa Mkataba (CEDAW)   | 3   |
| 2.3 Kupitishwa kwa Mkataba (CEDAW)   | 3   |
| 2.4 Makubaliano yaliyoainishwa na Mkataba (CEDAW)  | 3   |
| 2.4.1 Maudhui ya Mkataba   | 3   |
| <b>3.0 UTEKELEZAJI WA CEDAW NCHINI TANZANIA</b>  | 5   |
| 3.1 Kuingiza Misingi ya usawa kwa wanawake katika Katiba   | 5   |
| 3.2 Kutunga na kurekebisha Sheria mbalimbali   | 5   |
| 3.3 Kuweka mfumo wa kitaasisi kuhusu masuala ya wanawake   | 6   |
| 3.4 Elimu kwa wanawake   | 7   |
| 3.5 Mpango wa Elimu bure kwa shule za msingi na sekondari  | 7   |
| 3.6 Kampeni za Kujenga ulewa kwa Umma kuhusu haki za wanawake na watoto                                      | 7   |
| <b>4.0 MIKATABA MINGINE INAYOLINDA HAKI ZA WANAWAKE</b>  | 7   |
| <b>5.0 HITIMISHO</b>   | 8   |

|   |    |
|---|----|
| <b>SURA YA PILI</b>   | 9  |
| TAFSIRI YA MKATABA WA KIMATIFA WA KUTOKOMEZA AINA ZOTE ZA   |    |
| UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE   | 9  |
| <b>UTANGULIZI</b>   | 9  |
| <b>SEHEMU YA I</b>  | 10 |
| Ibara ya 1: Tafsiri   | 10 |
| Ibara ya 2: Hatua za Kisera na Kisheria   | 10 |
| Ibara ya 3: Hatua za kuleta Usawa katika nyanja zote za kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisheria | 10 |
| Ibara ya 4: Hatua mahsusizi za muda kuharakisha Haki ya Usawa   | 10 |
| Ibara ya 5: Hatua za kuondoa mila na desturi kandamizi  | 10 |
| Ibara ya 6: Hatua za kuzuia Usafirishaji Wanawake na Ukahaba  | 10 |
| <b>SEHEMU YA II</b>   | 11 |
| Ibara ya 7: Hatua za kuhakikisha Haki katika Shughuli za Umma   | 11 |
| Ibara ya 8: Hatua za kuleta Usawa katika Uwakilishi Kimataifa   | 11 |
| Ibara ya 9: Hatua za Usawa wa Uraia   | 11 |
| <b>SEHEMU YA III</b>  | 11 |
| Ibara ya 10: Hatua za Usawa katika Elimu  | 11 |
| Ibara ya 11: Hatua za Usawa katika Ajira  | 12 |
| Ibara ya 12: Hatua za Usawa katika Huduma za Afya   | 12 |
| Ibara ya 13: Hatua za Usawa Kiuchumi  | 12 |
| Ibara ya 14: Hatua za kuleta Usawa kwa Wanawake wa Vijijini   | 12 |
| <b>SEHEMU YA IV</b>   | 13 |
| Ibara ya 15: Hatua za kuleta Usawa mbele ya Sheria  | 13 |
| Ibara ya 16: Hatua za Usawa katika masuala ya Ndoa na Familia   | 13 |
| <b>SEHEMU YA V</b>  | 14 |
| Ibara ya 17: Kamati ya kusimamia Utekelezaji wa Mkataba na Muundo wake                                      | 14 |
| Ibara ya 18: Uwasilishaji Taarifa za Utekelezaji wa Mkataba   | 14 |
| Ibara ya 19: Kanuni za uendeshaji shughuli za Kamati  | 14 |
| Ibara ya 20: Mikutano ya Kamati   | 14 |
| Ibara ya 21: Taratibu za Kamati kuwasilisha Taarifa   | 15 |
| Ibara ya 22: Ushiriki wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa  | 15 |
| <b>SEHEMU YA VI</b>   | 15 |
| Ibara ya 23: Masharti ya Mkataba kutoathiri Sheria za Nchi Wanachama  | 15 |
| Ibara ya 24: Hatua za kulinda Haki za Wanawake  | 15 |
| Ibara ya 25: Mkataba kusainiwa na kuridhiwa   | 15 |
| Ibara ya 26: Maombi ya kuupitia Mkataba   | 15 |
| Ibara ya 27: Mkataba kuanza kutumika  | 15 |
| Ibara ya 28: Maelezo ya kutofungwa na baadhi ya Ibara za Mkataba  | 15 |
| Ibara ya 29: Utatuzi wa Migogoro kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba                                      | 16 |
| Ibara ya 30: Mkataba kuhifadhiwa katika Lugha rasmi   | 16 |
| <b>KIAMBATISHO: CONVENTION ON THE ELIMINATION OF ALL FORMS OF DISCRIMINATION AGAINST WOMEN</b>              | 16 |
| <b>MAREJEO</b>  | 25 |

# **SURA YA KWANZA**

## **UFAFANUZI NA UTEKELEZAJI WA MKATABA NCHINI TANZANIA**

**1.0**

### **UTANGULIZI**

Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka 1979 (The Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women – CEDAW) ulipitishwa Jijini New York, Marekani kwa Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Namba 34/180 tarehe 18 Disemba, 1979. Mkataba huu unabainisha wajibu mahsus kwa nchi wanachama katika kuhakikisha kuwa wanawake wanapata haki zote za binadamu kwa usawa na wanaume kwa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.

Aidha, Mkataba umefafanua ubaguzi kuwa ni utofautishaji, utengaji au katazo kwa misingi ya jinsi kunakoathiri wanawake, bila kujali hadhi yao ya ndoa, katika kupata haki za msingi za binadamu kwa usawa na wanaume katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na nynginezo.

Kwa kuridhia au kukubali Mkataba huu, nchi wanachama zinakubali wajibu wa kuweka usawa kati ya wanaume na wanawake katika mfumo wake wa kisheria na kitaasisi. Aidha, nchi wanachama zinawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba kila baada ya miaka minne.

Aidha, Mkataba huu unaweka masharti ya wajibu kwa Nchi Wanachama tu katika kuhakikisha kuwa wanawake wanapata haki kwa usawa bila kuainisha haki hizo. Kwa msingi huo, Mkataba huu unapaswa kuzingatiwa katika misingi ya haki za binadamu sambamba na mikataba na hati nyngine za kisheria kuhusu haki za binadamu kwa ujumla.

#### **1.1 Msingi wa Haki za Binadamu**

Haki za binadamu ni haki ambazo binadamu yoyote anastahili kuwa nazo tangu anapozaliwa bila kujali jinsi au kigezo kingine chochote kwa kuwa ni za asili kwa utu wa binadamu. Haki hizi ni kama vile haki ya kuishi, haki ya usawa, haki ya uhuru wa mawazo, haki ya kwenda mahali popote na haki ya kujihifadhi ikiwa ni pamoja na faragha.

Kwa msingi huu, siyo lazima haki za msingi za binadamu ziainishwe kwenye mkataba wa kimataifa au kwenye hati nyngine yoyote ya kisheria ili mtu aweze kuzipata. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza duniani hususan madhila ya vita ya kwanza na vita ya pili ya dunia, Jumuiya ya Kimataifa iliona umuhimu wa kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha haki za msingi za binadamu zinaendelezwa na kulindwa ipasavyo.

#### **1.2 Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu**

Makubaliano mbalimbali ya kimataifa kuhusu haki za binadamu yalipitishwa na kuridhiwa ili kulinda haki za binadamu duniani kote. Yafuatayo ndiyo makubaliano ya msingi katika masuala yote yanayohusu haki za binadamu duniani:

##### **1.2.1 Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 (The Universal Declaration of Human Rights, 1948)**

Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 limekubaliwa na kuperitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Disemba, mwaka 1948. Tamko hili linajumuisha aina zote za haki za binadamu, yaani haki za kiraia na kisiasa pamoja na haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Tamko hili linachukuliwa kuwa ndiyo tafsiri na ufanuzi rasmi wa viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Aidha, tamko hili ndiyo kielelezo kikuu cha viwango vya haki za binadamu kwa kila nchi na hivyo kuwa na uzito hata kwa nchi ambazo hazijaweka mfumo thabiti wa kuendeleza na kulinda haki za binadamu.

Licha ya hivyo, Tamko hili lina mapungufu ya kukosa misingi ya kisheria ya kuzibana nchi wanachama kutekeleza haki za binadamu. Hata hivyo, tamko hili lina heshima kubwa kimataifa ambapo nchi nyngi duniani zimelitambua na kuingiza misingi ya tamko hili kwenye katiba zao. Mathalan, Tanzania imeainisha misingi hiyo katika Ibara ya 9 (f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kutokana na Tamko hili kukosa nguvu ya kisheria, mwaka 1966 jumuiya ya kimataifa kuperitia

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa iliamua kupertisha mikataba miwili ya msingi kwa ajili ya kuendeleza na kulinda haki za binadamu kisheria. Mikataba hiyo ni Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966 (International Covenant on Civil and Political Rights of 1966) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966 (International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights of 1966).

### **1.2.2 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa Mwaka 1966**

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ulipitishwa tarehe 16 Disemba, 1966 na kuanza kutumika tarehe 23 Machi, 1976. Haki za kiraia na kisiasa zilizoainishwa katika Mkataba huu ni:

- i) Haki ya kuishi, ukamilifu, uhuru na usalama wa mtu;
- ii) Haki mbele ya vyombo veya sheria;
- iii) Haki ya faragha;
- iv) Haki ya kuabudu dini au imani;
- v) Haki ya kutoa maoni na kujieleza;
- vi) Haki ya mtu kwenda kokote na makazi;
- vii) Haki ya kukusanyika na kujunga kwenye kikundi au chama chochote;
- viii) Haki ya kushiriki katika masuala ya kisiasa; na
- ix) Haki ya uhuru wa mawazo.

Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1976 na kuzianisha haki hizi katika Sura ya Kwanza, Sehemu ya Tatu (Ibara za 12 hadi 32) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

### **1.2.3 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966**

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa ulipitishwa tarehe 16 Disemba 1966 na kuanza kutumika tarehe 3 Januari 1976. Mkataba huu unajumuisha haki zifuatazo:

- i) Haki ya kufanya kazi katika mazingira mazuri ya kazi;
- ii) Uhuru wa kuwa au kujunga kwenye vyama veya wafanyakazi;
- iii) Haki ya kiwango cha kutosheleza cha maisha (ikiwemo chakula, mavazi na malazi);
- iv) Haki ya afya, kupumzika, burudani na starehe;
- v) Haki ya elimu; na
- vi) Haki ya kushiriki katika maisha ya kiutamaduni ya jamii inayomhusu.

Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1976 na kuzianisha haki hizi katika Ibara ya 11 pamoja na Sura ya Kwanza, Sehemu ya Tatu (Ibara ya 12 hadi 32) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

### **1.2.4 Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Makundi Mbalimbali**

Pamoja na uwepo wa Mikataba iliyopitishwa na kuridhiwa kuhusu haki za binadamu, jumuiya ya kimataifa iliona kuna umuhimu wa kuainisha na kutambua haki za makundi mbalimbali kama vile wanawake, watoto, wazee na kundi la watu wenye ulemavu. Miiongoni mwa Mikataba iliyopitishwa katika kutambua haki za makundi hayo ni Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka 1979.

## **2.0 MKATABA WA KIMATAIFA WA KUTOKOMEZA AINA ZOTE ZA UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE WA MWAKA 1979**

Kwa kuzingatia asili na misingi ya haki za binadamu, wanawake na wanaume wana haki sawa lakini kutokana na sababu mbalimbali, wanawake hawakuweza kupata haki zao kwa usawa na wanaume. Hivyo, ili kuhakikisha wanawake wanapata haki sawa na wanaume Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka 1979

### **2.1 Chimbuko la Mkataba (CEDAW)**

Mkataba huu ultokana na kuundwa kwa Tume ya Kimataifa ya Kufuatilia Hadhi ya Wanawake (Commission on the Status of Women – CSW) mnamo tarehe 21 Juni, 1946 kwa kupertisha mchakato ufuatao:

#### **2.1.1 Hatua zilizochukuliwa na Tume**

Jukumu la msingi la Tume hii ni kutoa mapendekezo kwa Baraza la Kimataifa la Masuala ya

Kiuchumi na Kijamii kuhusu uendelezaji wa haki za wanawake katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu pamoja na masuala yote ya dharua kwa wanawake katika nyanja hizo. Kwa kipindi cha mwaka 1949 hadi 1959, Tume ilipendekeza na kupitishwa kwa Mikataba na hati za kisheria zifuatazo:

- i) Mkataba wa Haki za Kisiasa za Wanawake wa mwaka, 1952 (The Convention on the Political Rights of Women, adopted by the General Assembly on 20th December 1952);
- ii) Mkataba wa Utaifa wa Wanawake Walioolewa wa mwaka 1957 (The Convention on the Nationality of Married Women, adopted by the Assembly on 29th January 1957);
- iii) Mkataba kuhusu Ridhaa ya Kuolewa, Umri wa chini wa Kuolewa na Usajili wa Ndoa wa mwaka 1962 (The Convention on Consent to Marriage, Minimum Age for Marriage and Registration of Marriages adopted on 7th November 1962); na
- iv) Mapendekezo kuhusu Ridhaa ya Kuolewa, Umri wa chini wa Kuolewa na Usajili wa Ndoa ya mwaka 1965 (The Recommendation on Consent to Marriage, Minimum Age for Marriage and Registration of Marriages adopted on 1st November 1965).

## 2.2 Mchakato wa Kutungwa kwa Mkataba (CEDAW)

Pamoja na Mikataba iliyotokana na mapendekezo ya Tume kulinda na kuendeleza haki za wanawake, Tume ilibaini kuwa Mikataba na mapendekezo hayo hayaku jitosheleza, hususan katika kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake.

Kutokana na mapungufu yaliyobainika, mwaka 1963 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilielekeza kuandaliwa kwa tamko litakalojumiisha mikataba na mapendekezo yote yanayohusu haki za wanawake katika hati moja ya kisheria. Hatua hiyo ilisababisha kupitishwa kwa Tamko la Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake la mwaka 1967 ambalo, hata hivyo, halikuwa na nguvu ya kisheria. Aidha, tamko hilo lilionekana kuwa na mapungufu makubwa katika utekelezaji kuhusu masuala ya usawa katika ndoa, familia na ajira.

Tume ya Kimataifa ya Kufuatilia Hadhi ya Wanawake ilifanya kazi mapungufu yaliyobainika ambapo mwaka 1972 Tume hiyo ilipendekeza kupitishwa kwa mkataba utakaokuwa na nguvu ya kisheria kuhusu haki za wanawake. Hivyo, Umoja wa Mataifa ulianzisha mchakato wa kupitishwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake.

## 2.3 Kupitishwa kwa Mkataba (CEDAW)

Mkataba huo ulipitishwa kwa ajili ya kuanza kusainiwa, kuridhiwa na kukubaliwa kwa Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Namba 34/180 la tarehe 18 Disemba, 1979. Aidha, Mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 3 Septemba, 1981 baada ya nchi ya ishirini kuridhia na kuwasilisha Hati Idhimi (Instruments) kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Tanzania ilisaini tarehe 17 Julai, 1980 na kuuridhia Mkataba huu mnamo tarehe 20 Agosti, 1985.

## 2.4 Makubaliano yaliyoainishwa na Mkataba (CEDAW)

Kama ilivyoeleza awali, lengo kuu la Mkataba huu ni kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake duniani. Hivyo, Mkataba huu umeandikwa kwa mfumo wa kuweka wajibu kwa nchi wanachama kutekeleza masharti hususan kwenye masuala ambayo yameainishwa katika **Ibara ya 2** ya Mkataba kuwa ni:

- a) Kuingiza kanuni ya usawa kwa wanawake katika katiba na sheria.
- b) Kuweka sheria na adhabu pale inapobidi ili kukataza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.
- c) Kulinda haki za wanawake kwa msingi ya usawa.
- d) Kufuta sheria zote zinazobagua wanawake.
- e) Kupitisha sheria, kurekebisha, kufuta sheria, mila na desturi zinazochangia kuleta ubaguzi dhidi ya wanawake.

### 2.4.1 Maudhui ya Mkataba

Maudhui ya Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake ni kama ifuatavyo:

- i) **Ibara ya 1** inatoa tafsiri ya ubaguzi dhidi wanawake ili kuweka usawa kati ya wanaume na wanawake kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni kiraia au nyanja nyingine.
- ii) **Ibara ya 2** inainisha hatua za kisera na kisheria zinazopaswa kuchukuliwa na Nchi Wanachama katika kuhakikisha kuwa wanawake wanalindwa na kupata haki sawa na wanaume.

- iii) **Ibara ya 3** Nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kuwa wanawake wanaendelezwa na kujengewa uwezo ili waweze kupata haki za msingi za binadamu.
- iv) **Ibara ya 4** inatoa fursa kwa Nchi Wanachama kuchukua hatua maalum za muda mfupi katika kuendeleza na kulinda haki ya usawa kwa wanawake wakati ikiweka mkakati wa kutekeleza malengo ya Mkataba.
- v) **Ibara ya 5** imemainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Nchi Wanachama katika kuondoa mila na desturi kandamizi dhidi ya wanawake na kujenga uelewa kuhusu wajibu wa mwanaume na mwanamke katika uzazi na makuzi ya watoto.
- vi) **Ibara ya 6** Nchi Wanachama kuchukua hatua stahiki ili kuzuia biashara haramu ya usafirishaji wanawake na ukahaba.
- vii) **Ibara ya 7** Nchi Wanachama kuchukua hatua za kuhakikisha wanawake wanashiriki sawa na wanaume katika shughuli za kisiasa na kijamii.
- viii) **Ibara ya 8** Nchi Wanachama kuchukua hatua zitakazowezesha wanawake kupata fursa sawa na wanaume za kushiriki na kuwakilisha serikali zao katika vyombo vya kimataifa.
- ix) **Ibara ya 9** Nchi Wanachama kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume kuchagua uraia wao na uraia wa watoto wao.
- x) **Ibara ya 10** Nchi Wanachama kuchukua hatua zitakazoweka usawa kati ya wanaume na wanawake katika masuala yote yanayohusu elimu.
- xi) **Ibara ya 11** Nchi Wanachama kuchukua hatua zitakazotoa haki kwa wanawake na kuweka usawa kati ya wanaume na wanawake katika masuala yote yanayohusu ajira, ujira na usalama mahali pa kazi.
- xii) **Ibara ya 12** Nchi Wanachama kuchukua hatua zitakazoweka usawa kati ya wanaume na wanawake katika masuala yote yanayohusu huduma ya afya.
- xiii) **Ibara ya 13** Nchi Wanachama kuchukua hatua zitakazoweka usawa kati ya wanaume na wanawake katika masuala ya kiuchumi na kijamii.
- xiv) **Ibara ya 14** Nchi Wanachama kuchukua hatua za makusudi kuondoa ubaguzi katika nyanja zote dhidi ya wanawake wanaishi vijijini.
- xv) **Ibara ya 15** Nchi Wanachama kutoa haki sawa kwa wanaume na wanawake katika masuala ya sheria.
- xvi) **Ibara ya 16** Nchi Wanachama kuchukua hatua zinazofaa kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake katika masuala yote yanayohusu ndoa na mahusiano ya kifamilia.
- xvii) **Ibara za 17** Kamati ya kusimamia utekelezaji wa Mkataba pamoja na muundo wake
- xviii) **Ibara ya 18** inaainisha utaratibu za kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mkataba.
- xix) **Ibara ya 19** inaainisha kanuni na utaratibu wa kuendesha shughuli za Kamati na upatikanaji wa uongozi wa Kamati.
- xx) **Ibara ya 20** inaeleza kuhusu muda na mahali ambapo mikutano ya Kamati itafanyika.
- xxi) **Ibara ya 21** inaeleza kuhusu uwasilishaji wa taarifa za Kamati kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kufafanua namna zitakavyofanyiwa kazi.
- xxii) **Ibara ya 22** inatoa fursa kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kushiriki katika tathmini na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkataba maeneo yanayoangukia katika wigo wa majukumu yao.
- xxiii) **Ibara ya 23** inaeleza kuwa masharti ya Mkataba hayataathiri mafanikio yaliyopo katika sheria za Nchi Wanachama au katika Mikataba ya Kimataifa ya kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake.
- xxiv) **Ibara ya 24** inaweka masharti kwa Nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha haki za wanawake kwa mujibu wa mkataba huu zinalindwa.
- xxv) **Ibara ya 25** inatoa fursa kwa Nchi yoyote kusaini na kuridhia Mkataba na kufafanua utaratibu wa kuhifadhi nyaraka za Mkataba
- xxvi) **Ibara ya 26** inatoa fursa kwa Nchi Wanachama kuwasilisha maombi ya kuupitia Mkataba kwa ajili ya kuuboresha.
- xxvii) **Ibara ya 27** inaeleza kuhusu kuanza kutumika kwa Mkataba.

- xxviii) **Ibara ya 28** inaeleza kuhusu uwasilishaji wa maeleo ya Nchi Wanachama kutofungwa na masharti ya baadhi ya Ibara za Mkataba.
- xxix) **Ibara ya 29** inatoa ufanuzi wa utatuzi wa migogoro kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba mionganoni mwa Nchi Wanachama.
- xxx) **Ibara ya 30** inataja kuwa Mkataba utahifadhiwa katika lugha 6 rasmi zilizodhibitishwa.

### **3.0 UTEKELEZAJI WA CEDAW NCHINI TANZANIA**

Tangu Mkataba wa CEDAW uliporidhiwa mnamo tarehe 20 Agosti, 1985, hatua mbalimbali zimechukuliwa na Tanzania katika kuutekeleza kwa mujibu wa matakwa ya Ibara ya 2 ya Mkataba. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:

#### **3.1 Kuingiza Misingi ya usawa kwa wanawake katika Katiba**

Tanzania imetekeleza matakwa ya Mkataba kwa kuweka misingi ya usawa kwa wanawake na wanaume kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 katika maeneo yafuatayo:

##### **(a) Haki za Binadamu**

Haki za binadamu zimeainishwa kwa usawa bila ubaguzi wa aina yoyote katika Sura ya Kwanza, Sehemu ya Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano (Ibara za 12 hadi 32) na katika Sura ya Tatu (Ibara za 11 hadi 25A) ya Katiba ya Zanzibar.

##### **(b) Ushiriki wa wanawake katika masuala ya siasa**

Katiba imezingatia haki ya usawa katika siasa kutokana na asili ya utamaduni wa jamii nyingi za Kitanzania. Kwa msingi huo, Ibara ya 66(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoea fursa ya kuwa na Wabunge wanawake wa viti maalum vyta uwakilishi Bungeni wasiopungua asilimia thelathini ya Wabunge wote.

Kwa upande wa Zanzibar, Katiba inatambua haki ya usawa kwa wanawake kushiriki katika siasa kwa kuweka nafasi za viti maalum kwa wanawake katika Baraza la Wawakilishi. Ibara ya 67(1) inabainisha kuwa, kutakuwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawake kwa idadi ya asilimia arobaini ya wajumbe wote wa kuchaguliwa katika majimbo ya uchaguzi.

Vilevile, Ibara ya 66(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaweza msingi kuwa katika idadi ya Wabunge kumi wanaoteuliwa na Rais, angalau Wabunge watano kati yao wanapswa kuwa wanawake.

### **3.2 Kutunga na kurekebisha Sheria mbalimbali**

Katika kutekeleza Mkataba wa CEDAW Tanzania imetunga na kurekebisha sheria mbalimbali ili kuondoa masharti ya kibaguzi dhidi ya wanawake. Marekebisho hayo yanalenga kuweka masharti ya usawa kati ya wanaume na wanawake katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:

##### **(a) Ajira**

Sheria na Kanuni mbalimbali kuhusu masuala ya ajira zilirekeblishwa ili kusisitiza sharti kuwa katika kuchagua na kuajiri (selection and recruitment) lazima kuzingatia usawa kati ya wanaume na wanawake. Mfano wa sheria hizo ni Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake pamoja na miongozo (Public Service Act, 2002, Public Service Regulations 2003, Public Employment Guideline na Public Service Scheme).

Aidha, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (the Employment and Labour Relations Act, 2004) katika kifungu cha 7 inaweza sharti la fursa sawa kwa wanawake na wanaume na kukataza ubaguzi wa aina yoyote mahali pa kazi. Vifungu vidogo vyta (4) na (5) vinaleza kuwa ni kosa la jinai kwa waajiri kufanya vitendo vyovypote vyenye kubagua wafanyakazi.

Vilevile, katika kifungu cha 10(2)(a) cha Sheria ya Ajira ya Zanzibar kinamtaka mwajiri kutoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake mahali pa kazi. Sheria hiyo pia ina kataza ubaguzi wowote mahali pa kazi.

##### **(b) Katazo la ubaguzi wa wanaume na wanawake kwa misingi mbalimbali**

Tanzania imetunga Sheria mbalimbali kama vile Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI (The Prevention of HIV/AIDS Act, 2008) ambayo inakataza ubaguzi kwa misingi ya ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, Sheria ya Watu wenye Ulemavu (The Persons with Disabilities Act, 2010) ambayo inakataza ubaguzi kwa misingi ya ulemavu.

Vilevile, Sheria ya Mtoto (The Law of the Child Act, 2009) na Sheria ya Watoto ya Zanzibar (Zanzibar Children's Act, 2011) zote zinakataza ubaguzi katika malezi ya watoto ambapo hapo awali jukumu hilo lilikuwa linafanywa na wanawake peke yao. Aidha, sheria hii imeweka masharti ya kuhakikisha haki za mtoto wa kike zinalindwa ikiwa ni pamoja na kupata elimu kwa kuzuia ndoa za utotonii.

**(c) Sheria ya Kanuni za Adhabu (The Penal Code, Cap. 16)**

Hii ni mionganini mwa Sheria iliyofanyiwa marekebisho ya msingi ili kuweka kosa la ukeketaaji kwa wanawake (Female Genital Mutilation) na kutambua kuwa unyanyasaji wa aina yoyote dhidi ya wanawake ni kosa la jinai.

**(d) Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana (Sexual Offences (Special Provisions) Act, 1998)**

Mwaka 1998 Bunge lilipitisha Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana (Sexual Offences (Special Provisions) Act, 1998) kwa lengo la kulinda hadhi ya wanawake katika jamii. Kimsingi, sheria ya Makosa ya Kujamiiiana imefanya mabadiliko katika sheria tano ambazo zinahusiana moja kwa moja na makosa ya kujamiiiana ambazo ni:

- i) Sheria ya Kanuni za Adhabu (The Penal Code, Cap. 16);
- ii) Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai (The Criminal Procedure Act, 1985);
- iii) Sheria ya Ushahidi ya (The Evidence Act, 1967);
- iv) Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo (The Children and Young Persons Act, Cap. 13 ambayo kwa sasa imefutwa na Sheria ya Mtoto, 2009); na
- v) Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu (The Minimum Sentences Act, 1972).

**(e) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, 2008 (The Anti-Trafficking in Persons Act, 2008)**

Kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, 2008 nchini ni mojawapo ya hatua za kutekeleza Mkataba huu. Sheria hii inaendana na masharti ya Ibara ya 6 ya Mkataba inayozitaka nchi wanachama kuchukua hatua madhubuti za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu na ukahaba.

**(f) Sheria ya Huduma za Msaada wa Kisheria, 2017 (The Legal Aid Act, 2017)**

Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 ilitungwa ili kuweka mfumo wa kisheria wa kutoa, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa mashauri ya jinai na madai kwa watu wasioyeza wa kumudu gharama za huduma za kisheria kwa malipo. Pamoja na mambo mengine, sheria hii inatoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake wanaishi vijiji kupata haki kama inavyotakiwa na Ibara ya 14 ya Mkataba.

### **3.3 Kuweka mfumo wa kitaasisi kuhusu masuala ya wanawake**

Tanzania imeanzisha taasisi mbalimbali ambazo pamoja na mambo mengine, zinasimamia na kuhamasisha utekelezaji wa Mkataba kama ifuatavyo:

**(a) Kuundwa kwa Wizara inayosimamia Masuala ya Jinsia**

Tanzania imekuwa ikidumisha utaratibu wa kuwa na Wizara inayosimamia masuala ya jinsia. Wizara hii imekuwa na jukumu la kuratibu, kutekeleza na kusimamia masuala yote yanayohusu haki za wanawake. Mpaka Oktoba 2018 Wizara inayosimamia eneo hili ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**(b) Kutunga Sera kuhusiana na Masuala ya Wanawake**

Tanzania imetunga Sera ya Jinsia (National Gender Policy) inayoelekeza kila taasisi ya Umma, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuunda vyombo vitakavyotekeliza Mkataba wa CEDAW na Nyongezaya (Protocol) kwa kuunda Kamati za masuala ya jinsia. Aidha, Sera ya utoaji bure wa huduma ya afya ilitungwa ili kusimamia huduma hiyo kwa wanawake wajawazito na watoto.

**(c) Kuanzisha madawati ya jinsia na watoto**

Madawati ya jinsia na watoto yanasiyamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika vituo vya polisi nchini. Lengo la kuanzisha madawati hayo ni kushughulikia malalamiko kuhusu vitendo vya unyanyasaji. Madawati hayo yanaratibiwa na wataalamu waliopata mafunzo kuhusu masuala ya jinsia na watoto. Aidha, uwepo wa madawati haya unatoa fursa muhimu kwa wanawake wanaokabiliwa na vitendo vya unyanyasaji kutafuta haki zao.

**(d) Asasi za kiraia**

Tanzania imeweka mfumo wa kisheria wa uanzishaji na uendeshaji wa taasisi zisizo za kiserikali. Kupitia fursa hii, baadhi ya Taasisi hizo zimeanzishwa kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha umma pamoja na kuendesha kampeni za kupambana na unyanyasaji dhidi ya wanawake. Vilevile taasisi hizo hutoa mchango katika kufanya tathimini na kufuutilia utekelezaji wa Mkataba. Zifuatazo ni baadhi ya taasisi

hizo:

- i) The Tanzania Women Parliamentary Group (TWPG)
- ii) Association for the Prevention of Torture (APT)
- iii) Campaign on Good Governance (CGG)
- iv) Feminist Activism (FEMACT)
- v) Taaluma Women Group (TWG)
- vi) Legal and Human Rights Centre (LHRC)
- vii) Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)
- viii) Women's Legal Aid Centre (WLAC)
- ix) Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)
- x) Women in Law and Development in Africa (WiLDAF)

### **3.4 Elimu kwa wanawake**

Katika kutekeleza Malengo wa Milenia kuhusu elimu, Tanzania iliongeza udahili kwa watoto wa kike katika ngazi mbalimbali za elimu. Mfano, kutoa kipaumbele katika mikopo ya elimu ya juu kwa watoto wa kike ili kupunguza tofauti kati ya wanawake na wanaume katika elimu.

### **3.5 Mpango wa Elimu bure kwa shule za msingi na sekondari**

Serikali ya awamu ya Tano imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari. Mpango huu unatoa fursa kwa watoto wengi kupata elimu ikiwemo watoto wa kike.

### **3.6 Kampeni za Kujenga uelewa kwa Umma kuhusu haki za wanawake na watoto**

Katika kutekeleza Mkataba, elimu kuhusu haki za wanawake na watoto imekuwa ikitolewa kwa makundi mbalimbali kama vile watumishi wa umma na sekta binafsi. Aidha, miongoni mwa njia zinazotumika kutoa elimu ni semina, mikutano, makongamano na kupitia vyombo vya habari. Mfano, wa vipindi vinavyorushwa kupia vyombo vya habari ni;

- (a) Ijue Sheria (ITV),
- (b) Kona ya Sheria (TBC 1),
- (c) Kumepambazuka –Sheria (Radio One),
- (d) Wanawake Live (EATV)
- (e) Nitetee (Star TV)
- (f) Wanawake katika Uongozi (TBC1), nk.

Vilevile, Serikali iliendesha kampeni ya kutokomeza kabisa unyanyasaji dhidi ya wanawake “DECLARE ZERO TOLERANCE NOW” kwa lengo la kujenga uelewa na kutafuta suluhu ya kutokomeza unyanyasaji huo.

## **4.0 MIKATABA MINGINE INAYOLINDA HAKI ZA WANAWAKE**

Katika kulinda na kuendeleza haki ya usawa kati ya wanawake na wanaume Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mingine mbalimbali ya kimataifa ambayo baadhi ni:

- (a) Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Ubaguzi katika Ajira na Eneo la Kazi wa mwaka (The Convention on the Elimination of Discrimination in Employment and Occupation, 1958);
- (b) Mkataba wa Kimataifa wa Usawa katika Ajira na Ujira kwa Kazi (The Convention on Equal Remuneration for work of Equal Value, 1951);
- (c) Mkataba wa Kimataifa wa Wafanyakazi wenye Majukumu ya Familia wa mwaka 1981 (The Convention on Workers with Family Responsibilities, 1981);
- (d) Mkataba wa Kimataifa wa kuhusiana na Masuala ya Uzazi wa mwaka 2000 (The Convention on Maternity Protection, 2000);
- (e) Maazimio ya Mkutano wa Kimataifa wa Wanawake uliofanyika Beijing mwaka 1995 (The Beijing Platform for Action 1995);
- (f) Maazimio ya Mkutano wa Kimataifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo mwaka 1994 (The Integrated Conference on Population and Development Plan of Action 1994);
- (g) Tamko la Milenia la mwaka 2000 (The Millennium Declaration, 2000);
- (h) Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 kuhusu Haki za Wanawake ya mwaka 2003 (The Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights (ACPHR) on the Rights of Women in Africa (2003)).

- (i) Tamko la Usawa wa Kijinsia Afrika chini ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 (The Declaration on Gender Equality in Africa, the African Charter on Human and Peoples' Rights, 1981);
- (j) Tamko kuhusu Janga la VVU/UKIMWI katika Mkutano wa Kimataifa kuhusu UKIMWI na Magonjwa ya Zinaa Afrika la mwaka 1999 (The Declaration on the HIV/AIDS Epidemic at the XI International Conference on AIDS and STDs in Africa 1999);
- (k) Tamko la Wanawake na Ajenda kuhusu Utamaduni na Amani Afrika la mwaka 1999 (The Women's Declaration and Agenda for a Culture of Peace in Africa adopted at the close of a Pan African Conference in Zanzibar in 1999);
- (l) Tamko la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Arika kuhusu Jinsia na Maendeleo la mwaka 1997 (The SADC Declaration on Gender and Development, 1997)

## 5.0 HITIMISHO

Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa Mwaka 1979 ni mojawapo ya hati muhimu za kisheria katika kulinda na kuendeleza haki za wanawake pamoja na kuleta usawa katika jamii. Masharti ya Mkataba huu yanapaswa kuzingatiwa sambamba na Tamko la Haki za Binadamu Duniani la mwaka 1948 pamoja na Mikataba ya Haki za Binadamu ya mwaka 1966 ambayo imeweka misingi mikuu ya uzingatiaji wa haki za binadamu duniani.

Tangu kusaini na kuridhia Mkataba wa CEDAW Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za utekelezaji ili kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume. Hatua hizo zinadhishirika katika sheria mbalimbali na uwepo wa taasisi zinazosimamia masuala ya wanawake kupata haki sawa na wanaume.

# **SURA YA PILI**

## **TAFSIRI YA MKATABA WA KIMATAIFA WA KUTOKOMEZA AINA ZOTE ZA UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE**

Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake Ulipitishwa kwa ajili ya kuanza kusainiwa, kuridhiwa na kukubaliwa kwa Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Namba 34/180 la tarehe 18 Disemba, 1979 Ulianiza kutumika rasmi tarehe 3 Septemba, 1981, kwa mujibui wa Ibara ya 27(1)

### **UTANGULIZI**

Nchi Wanachama kwa Mkataba huu, Kwa kutambua kuwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa unasisitiza uaminifu katika haki za msingi za binadamu, utu na thamani ya mtu na katika usawa wa haki za wanaume na wanawake,

Kwa kutambua kwamba Tamko la Dunia la Haki za Binadamu linasisitiza kanuni ya kukataa ubaguzi na kutamka kuwa binadamu wote wamezaliwa huru na kwa usawa katika utu na haki na kwamba kila mmoja anastahili haki zote na uhuru kama zilivyoainishwa katika Tamko hilo, bila kuweka tofauti ya aina yoyote, ikiwemo kuweka tofauti kwa kuzingatia jinsi,

Kwa kutambua kwamba Nchi Wanachama zilizoridhia Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu zina wajibu wa kuhakikisha haki sawa kwa wanaume na wanawake katika kupata haki zote za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa,

Kwa kuzingatia kwamba Mikataba ya Kimataifa iliyopitishwa chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa na Mashirika yake mahsusui inakuza usawa wa haki za wanaume na wanawake,

Kwa kuzingatia kwamba maaazimio, matamko na mapendekezo yaliyopitishwa na Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa katika kuhimiza haki sawa baina ya wanaume na wanawake

Kwa kuzingatia, hata hivyo, kwamba licha ya uwepo wa Mikataba hii bado ubaguzi mkubwa dhidi ya wanawake unaendelea kuwepo,

Kwa kutambua kwamba ubaguzi dhidi ya wanawake unakiuka misingi ya usawa wa haki na heshima ya utu wa binadamu ni kikwazo cha ushiriki wa wanawake, kwa usawa na wanaume, katika nyanja za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni katika nchi zao, kunaathiri ustawi wa jamii na familia na kuleta ugumu katika kuwezesha wanawake kutumikia nchi zao na kujali ubinadamu,

Kwa kutambua kwamba katika hali ya umaskini wanawake wana nafasi finyu ya kupata mahitaji ya chakula, afya, elimu, mafunzo, fursa za ajira na mahitaji mengine,

Kwa kushawishika kwamba kuanzhishwa kwa mfumo mpya wa kimataifa wa kiuchumi unaozingatia usawa na haki kutachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza usawa kati ya wanaume na wanawake,

Kwa kusisitiza kwamba kuondoa mfumo wa ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini (Apartheid), aina zote za ubaguzi wa kimbari, ubaguzi wa rangi, ukoloni, ukoloni mamboleo, uvamizi wa nchi, utawala wa mabavu na kuingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine ni muhimu katika upatikanaji wa haki za wanaume na wanawake,

Kwa kuthibitisha kwamba kuimashwa kwa amani na usalama kimataifa, kupunguzwa kwa mizozo ya kimataifa, ushirikiano wa pamoja mionganii mwa mataifa bila kujali mifumo yao ya kijamii na kiuchumi, kuondoa matumizi ya nguvu za kijeshi hususan kutokomeza silaha za kinyuklia chini ya usimamizi mkali unaowekwa kimataifa, uthibitishaji wa kanuni za haki, usawa na manufaa ya pamoja katika mahusiano baina ya nchi na kutambua kuwa watu waliopo katika nchi zinazotawaliwa na nchi za kigeni, nchi zilizo chini ya ukoloni na zinazotawaliwa wana haki ya kujitawala na kuwa huru, pamoja na kuheshimu mamlaka ya taifa na kutovamia mipaka ya nchi nyingine, kutakuza maendelezo ya kijamii na hivyo kuchangia upatikanaji wa usawa kamili kati ya wanaume na wanawake,

Kwa kushawishika kwamba kunahitajika ushiriki wa hali ya juu wa wanawake kwa usawa na wanaume ili kupata maendeleo kamili ya nchi, usawa duniani na kuwepo kwa hali ya amani,

Kwa kuzingatia kuwa mchango mkubwa wa wanawake katika ustawi wa familia na maendeleo ya jamii hautambuliki ipasavyo, umuhimu wa uzazi kijamii na jukumu la wazazi wote katika familia na malezi ya watoto, na kwa kutambua kuwa jukumu la wanawake kuzaa halipaswi kuwa ndiyo msingi wa ubaguzi kwa kuwa malezi ya watoto yanahitaji kusaidiana majukumu kati ya wanaume, wanawake na jamii kwa ujumla,

Kwa kuelewa kwamba kunahitajika mabadiliko ya desturi iliyozoleka ya mgawanyo wa majukumu kati ya wanaume na wanawake katika jamii na familia ili kupata usawa kamili kati ya wanume na wanawake,

Kwa kukusudia kutekeleza kanuni zilizowekwa na Tamko la Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake na hivyo kuweka njia zinazohitajika kwa ajili ya kutokomeza ubaguzi huo na mambo mengine yote yanayoambatana na ubaguzi,

Zamekubaliana kama ifuatavyo:

## SEHEMU YA I

### Ibara ya 1: Tafsiri

Kwa madhumuni ya Mkataba huu, maneno “**ubaguzi dhidi ya wanawake**” yatakuwa na maana ya kutofautishwa, kutengwa au kuzuwa kwa namna yoyote kwa misingi ya jinsia kwa lengo la kudhoofisha au kubatilisha kutambuliwa, kufurahia au uwezo wa kutenda wa wanawake, bila kujali hadhi yao ya ndoa, kwa misingi ya usawa kati ya wanaume na wanawake, haki za kibinadamu na msingi ya uhuru wa asili wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia au eneo lolote lile.

### Ibara ya 2: Hatua za Kisera na Kisheria

Nchi Wanachama zinalaani ubaguzi dhidi ya wanawake katika aina zake zote, zinakubaliana kutunga na kutekeleza kwa njia zozote zile zinazofaa na bila kuchelewa, sera kwa ajili ya kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake na, katika kutimiza lengo hili, kufanya yafuatayo:

- Kuingiza dhana ya usawa wa wanaume na wanawake katika Katiba zao au katika sheria yoyote inayofaa endapo haki hiyo bado hajaingizwa, na kuhakikisha kuwa, kupitia sheria na njia nyingine zinazofaa haki ya usawa kati ya wanaume na wanawake inatekelezwa ipasavyo;
- Kuchukua hatua muhimu za kisheria au hatua nyinginezo zinazofaa, ikiwa ni pamoja na kuweka adhabu inapobidi, ili kuzuia ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake;
- Kuanzisha ulinzi wa kisheria wa haki za wanawake kwa misingi ya usawa kati yao na wanaume na kuhakikisha kuwa kwa kupitia mahakama zenye mamlaka za nchi na taasisi nyingine za umma zinazohusika kuna ulinzi imara kwa wanawake dhidi ya vitendo vya ubaguzi;
- Kutojihusisha na vitendo vyovoye vile au mila na tamaduni za ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha kuwa mamlaka za umma na taasisi zinatekeleza majukumu kwa kuzingatia wajibu huu;
- Kuchukua hatua zote zinazofaa kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake unaofanywa na mtu yejote, taasisi au kampuni binafsi;
- Kuchukua hatua zote zinazofaa, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria, kurekebisha au kufuta sheria zilizopo, kanuni, tamaduni, mila na desturi zinazoendekeza ubaguzi dhidi ya wanawake.
- Kufuta vifungu vyote vya sheria zinazotoa adhabu ambavyo vina mianya ya ubaguzi dhidi ya wanawake.

### Ibara ya 3: Hatua za kuleta Usawa katika nyanja zote za kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisheria

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa katika nyanja zote, hususan kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni, zikiwemo za kisheria, kuhakikisha kuna maendeleo na ustawi kamili wa wanawake, kwa lengo la kuwahakikisha kuwa wananufaika na haki za binadamu na misingi ya uhuru kwa vigezo vya usawa kati yao na wanaume.

### Ibara ya 4: Hatua mahsusizi za muda kuharakisha Haki ya Usawa

- Nchi Wanachama zitachukua hatua mahsusizi za muda mfupi kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa haki ya sawa kati ya wanaume na wanawake, na jambo hilo halitachukuliwa kuwa ni ubaguzi kama ilivyotafsiriwa katika Mkataba huu, bali kwa namna yoyote ile hatua hizo hazitahusishwa na matokeo ya ukosefu wa usawa au viwango tofauti baina ya wanaume na wanawake; hatua hizi zitasitishwa endapo malengo ya fursa za usawa na utekelezaji wake vitakapopatikana.
- Nchi Wanachama kuchukua hatua mahsusizi, ikiwa ni pamoja na hatua zilizomo katika Mkataba huu kwa lengo la kulinda masuala ya uzazi, hayatatafsiriwa kuwa ni ubaguzi.

### Ibara ya 5: Hatua za kuondoa mila na desturi kandamizi

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa katika:

- Kurekebisha mifumo ya kijamii na kiutamaduni kuhusu mienendo ya wanaume na wanawake, kwa lengo la kuondoa madhara ya tamaduni au mila na desturi zenye misingi ya kutweza au kukuza jinsi moja ijisikie duni kuliko nyingine, au ijione bora kuliko nyingine kwa misingi ya mgawanyo wa majukumu ya kila mmoja.
- Kuhakikisha kwamba elimu ya familia inazingatia uelewa sahihi wa elimu ya uzazi kama jukumu la kijamii na kutambuliwa kuwa ni jukumu la pamoja kati ya wanaume na wanawake katika malezi, makuzi na maendeleo ya watoto wao, na ikieleweka kwamba maslahi ya watoto yanatakiwa kuzingatiwa na kupewa kipaumbele katika mazingira ya aina yoyote.

### Ibara ya 6: Hatua za kuzuia Usafirishaji Wanawake na Ukahaba

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote muhimu, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria, kuzuia aina zote za usafirisha haramu wa wanawake na unyonyaji wa wanawake kupitia vitendo vya ukahaba.

## **SEHEMU YA II**

### **Ibara ya 7: Hatua za kuhakikisha Haki katika Shughuli za Umma**

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake katika masuala ya kisiasa na maisha ya kijamii katika nchi zao, hususan, kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanapata haki zifuatazo:

- (a) Kupiga kura katika chaguzi zote na kura za maoni na kuwa na sifa za kugombea na kuchaguliwa kwenye vyombo vyote vya umma vya kiuchaguzi;
- (b) Kushiriki katika kutunga sera za serikali na utekelezaji wake na kushika madaraka katika ofisi za umma na kutekeleza majukumu ya umma katika ngazi zote serikalini;
- (c) Kushiriki katika asasi zisizokuwa za kiserikali na vyama vingine vinavyohusika na maisha ya kijamii na kisiasa katika nchi.

### **Ibara ya 8: Hatua za kuleta Usawa katika Uwakilishi Kimataifa**

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kuwahakikishia wanawake kwa misingi iliyo sawa na wanaume, bila ubaguzi wowote, kuwa wanapata fursa ya kuwakilisha Serikali zao katika ngazi ya kimataifa na kushiriki katika shughuli za mashirika ya kimataifa.

### **Ibara ya 9: Hatua za Usawa wa Uraia**

1. Nchi Wanachama zitatoa haki sawa kwa wanawake na wanaume kupata, kubadilisha au kurudishiwa uraia wao. Zitahakikisha kimsingi kuwa kufunga ndoa na raia wa kigeni au mume kubadilisha uraia wakiwa kwenye ndoa haitabdalisha uraia wa mke, au kumfanya asiwe na uraia au kumlazimisha kuchukua uraia wa mume wake.
2. Nchi Wanachama zitatoa haki sawa kwa wanawake na wanaume kuhusu uraia wa watoto wao.

## **SEHEMU YA III**

### **Ibara ya 10: Hatua za Usawa katika Elimu**

Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake ili kuwahakikishia haki sawa na wanaume katika elimu, hususan, kuwahakikisha kuwa, katika misingi ya usawa wa wanaume na wanawake:

- (a) Mazingira sawa ya kazi na mwongozo wa mafunzo ya kitaalamu, fursa za masomo na kufuzu katika taasisi za elimu kwa aina zote za elimu katika maeneo ya vijiji ni mijini; usawa huu utazingatiwa katika ngazi za masomo ya awali, kawaida, ufundi, kitaaluma na ngazi ya elimu ya juu ya ufundi pamoja na aina zote za mafunzo ya kuongeza ujuzi na utaalamu wa kazi;
- (b) Fursa ya kupata mafunzo kwa kutumia mitaala sawa, kupewa mtihani sawa, kufundishwa na walimu wenye sifa na viwango sawa, na kusoma katika mazingira ya shule na vifaa vyenye ubora sawa;
- (c) Kutokomeza unyanyapaa kwa misingi ya majukumu kati ya wanaume na wanawake katika ngazi zote na katika aina zote za elimu kwa kusisitiza elimu kwa jinsi zote kwa pamoja na aina nyingine za elimu ambazo zitasaidia kufanikisha lengo hili, hususan, kufanya marejeo vitabu vya kiada na programu za shule na kutumia mbinu sahihi za ufundishaji;
- (d) Fursa sawa za kunufaika na ufadhilli wa masomo na misaada mengine ya kielimu;
- (e) Fursa sawa katika za kujijendeleza kielimu, ikiwa ni pamoja na elimu ya watu wazima na mpango wa elimu ya kujifunza kusoma na kuandika kwa watu wazima, hususan kwa lengo la kupunguza mapema iwezekanavyo pengo la kielimu kati ya wanaume na wanawake;
- (f) Kupunguza kiwango cha wanafunzi wa kike wanaoacha shule na kuweka mipango ya elimu kwa wasichana na wanawake walioacha shule mapema;
- (g) Fursa sawa ya kushiriki katika michezo na elimu ya mazoezi ya viungo;
- (h) Fursa ya kupata taarifa mahususi za kielimu ili kuhakikisha masuala ya afya na ustawi wa familia, pamoja na taarifa na ushauri kuhusu uzazi wa mpango.

### **Ibara ya 11: Hatua za Usawa katika Ajira**

1. Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake katika nyanja za ajira ili kuhakikisha, katika misingi ya usawa wa wanaume na wanawake, haki sawa hususan:
  - (a) Haki ya kufanya kazi kama haki stahili ya asili kwa binadamu wote;
  - (b) Haki sawa katika fursa za ajira, ikiwemo matumizi ya vigezo sawa vya uteuzi katika masuala ya ajira;
  - (c) Haki ya uhuru wa kuchagua taaluma na ajira, haki ya kupandishwa daraja, usalama wa kazi na marupurupu yote na mazingira mazuri ya kazi na haki ya kupata mafunzo ya kuongeza ujuzi na uthalamu kazini ya mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na mafunzo kazini, mafunzo ya elimu ya juu ya kitaalamu na mafunzo ya kujiendeleza mara kwa mara kazini;
  - (d) Haki ya kupata malipo sawa, ikiwa ni pamoja na marupurupu, na kupata manufaa mengine kazini kwa usawa na kwa thamani sawa, pamoja na usawa katika kupima tathmini ya kazi;
  - (e) Haki ya kupata huduma za hifadhi ya jamii, hususan mafao ya kustaafu, ukosefu wa ajira, ugonjwa, hali ya kukosa uwezo wa kufanya kazi na uzee, pamoja na likizo ya malipo;
  - (f) Haki ya ulinzi kiafya na usalama katika mazingira ya kazi, ikiwa ni pamoja na usalama katika uzalishaji mali;
2. Ili kuzuia ubaguzi dhidi ya wanawake kwa misingi ya ndoa au masuala ya uzazi na kuhakikisha ufanisi wa haki yao ya kufanya kazi, Nchi Wanachama zitachukua hatua muhimu zifuatazo:
  - (a) Kuzuia kufukuzwa kazini kwa sababu ya kupata ujauzito au likizo ya uzazi na kupiga marufuku ubaguzi wa kufukuzwa kazi kwa misingi ya hadhi ya ndoa, na kuweka adhabu kwa watakaokiuka masharti haya.
  - (b) Kuanzisha likizo ya malipo ya uzazi au yenze mafao ya hifadhi za kijamii bila kupoteza ajira, cheo, daraja au posho husika;
  - (c) Kuhimiza utolewaji wa huduma muhimu za kijamii kusaidia wazazi kuunganisha majukumu ya kifamilia pamoja na majukumu ya kazi na ushiriki katika shughuli za umma, hususan katika kukuza uanzishwaji na uendelezaji wa mtandao wa huduma za malezi ya watoto;
  - (d) Kutoa ulinzi mahsus kwa wanawake wakati wa ujauzito kwa aina ya kazi zilizothibitishwa kuwa na madhara kwoo;
3. Sheria zitakazotungwa kutoa ulinzi kwa wanawake katika masuala yaliyofafanuliwa katika ibara hii zitafanyiwa mapitio kila mara kwa vipindi maalum kwa muktadha wa ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia na hivyo zitafanyiwa maboresho, kufutwa au kupanuliwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

### **Ibara ya 12: Hatua za Usawa katika Huduma za Afya**

1. Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake katika eneo la huduma za afya ili kuhakikisha, katika misingi ya usawa baina ya wanaume na wanawake kuna fursa kwa huduma za kiafya, ikiwa ni pamoja na huduma zinazohusu uzazi wa mpango.
2. Bila ya kuathiri masharti ya aya ya 1 ya ibara hii, Nchi Wanachama zitawahakikishia wanawake huduma zinazofaa wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua, baada ya kujifungua, kutoa huduma bure pale inapobidi, na pia kutoa lishe ya kutosha wakati wa ujauzito na wakati wa kunyonyesha.

### **Ibara ya 13: Hatua za Usawa Kiuchumi**

